**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**(Kikao cha Nne - Tarehe 31 Machi, 2006)**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea naomba kutambua wageni mashuhuri walioko kwenye *gallery* ya Spika, ni Mheshimiwa Balozi wa Marekani Michael Ragizer akiwa amefuatana na Mkuu wa Sehemu ya Siasa na Uchumi, Mama Mary Johnson na msaidizi wa kisiasa Mama Justina Mdobilu. *(Makofi)*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):**

Taarifa ya mwaka ya Utendaji wa Soko la Bima Nchini kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2004 *(The Annual Insurance Market Performance Report for the year ended 31st December, 2004).*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 45

**Kugawanywa Wilaya ya Manyoni**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Kwa kuwa eneo la Wilaya nzima ya Manyoni ni sawa na asilimia 58 ya eneo lote la Mkoa wa Singida na kwa kuwa Jimbo la Manyoni Magharibi lina vigezo vyote vya kulifanya kuwa Wilaya:-

Je, ni lini Serikali itaigawa Wilaya ya Manyoni ili kuwahudumia wananchi wa Jimbo hilo kwa ukaribu na ufanisi zaidi ili kuharakisha maendeleo yao?

**NAIBU WAZIRI , OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uundaji na ugawaji wa maeneo mapya ya utawala hapa nchini unatawaliwa na sheria Na. 7 ambayo inahusika na Mamlaka za Wilaya na Sheria Na. 8 ambayo inashughulika na Mamlaka za Miji, zote za mwaka 1982 na sheria ya taratibu za uanzishwaji wa Mikoa na Wilaya Na. 12 ya mwaka 1994.

Mheshimiwa Spika, sambamba na sheria hii, vipo vigezo muhimu vinavyozingatiwa kabla ya kuanzisha Wilaya mpya. Wakati nilipokuwa najibu swali langu namba 13 lililoulizwa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby Mbunge wa Gairo tarehe 8 Februari, 2006 katika Mkutano wa pili wa Bunge kuhusu kugawa Wilaya ya Kilosa nilieleza kwamba vigezo ni kama hivi vifuatavyo:-

(i) Ukubwa wa eneo usiopungua kilometa za mraba 5,000;
(ii) Idadi ya Kata zisizopungua 15;
(iii) Idadi ya Tarafa zisizopungua 5;
(iv) Idadi ya Vijiji visivyopungua 50;
(v) Idadi ya watu wasiopungua 100,000; na
(vi) Eneo lenye jiografia ambayo inazuia huduma kuwafikia wananchi kwa urahisi kama vile milima, mito, misitu mikubwa na visiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia vigezo nilivyovitaja hapo juu, Wilaya ya Manyoni inakidhi baadhi ya vigezo ambavyo vingeweza kuifanya igawanywe kuwa Wilaya mbili. Kwa mfano, ukubwa wa eneo ni kilometa za mraba 28,620 na wakazi wapatao 204,482 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002. Wilaya ya Manyoni ina eneo kubwa lakini eneo kubwa zaidi ni hifadhi ya mapori ya akiba *(Game Reserve)* ya Rungwa, Mhesi na Kizigo lenye kilometa za mraba 12,815. Pia Wilaya ina Kata 21 na Tarafa 5 na Vijiji 78.

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumika kugawa Wilaya ni shirikishi kwa kawaida Wilaya yenyewe kwa kupitia vikao vya Baraza la Madiwani kuona haja ya kugawa Wilaya husika na kupitisha Azimio la kugawa Wilaya hiyo. Azimio hilo hupelekwa ngazi ya Mkoa na kufanyiwa tathmini na kuwasilishwa ngazi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inampa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka ya kugawa nchi kulingana na atakavyoona inafaa. Kwa mantiki hiyo yapo pia mambo mengine ya Kitaifa yanayoangaliwa kabla ya kuanzisha eneo jipya la utawala.

Mheshimiwa Spika, mambo hayo ni pamoja na gharama za uanzishaji na uendeshaji wa shughuli za utawala katika eneo husika. Napenda kulieleza Bunge lako Tukufu, kwamba pindi eneo linapokidhi baadhi ya vigezo na hali ya fedha inaporuhusu Rais wa Jamhuri hushauriwa kugawa eneo husika.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kwamba Jimbo la Manyoni Magharibi lina vigezo karibu vyote na sababu kubwa ambayo inatolewa imekuwa ikitolewa kwamba ni idadi ya watu. Kwa kuwa kulingana na sensa ya mwaka 2002 haikuwa makini kwa upande wetu kwa sababu ya mgogoro wa mpaka uliopo kati ya Sikonge na Wilaya ya Manyoni, Vijiji vya Kitagata, Mtakuja, Makale, Kayui, Mitundu, Kalangani hesabu zake hazikuwa sahihi.

Je, pindi itakapobainika kwamba tunakidhi vigezo hivyo vya idadi je, Naibu Waziri anaweza kunihakikishia kwamba ataiweka kwenye Bajeti ili tuwe Wilaya kamili? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge, kwamba tukianza kugawa Wilaya kwa kufuata Majimbo tutakuwa tumekiuka sheria namba 8 na sheria namba 7 za Serikali za Mitaa za mwaka 1982.

Pili, tutakuwa tumeingilia ugawaji wa Majimbo ambao hutekelezwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Tume ya Taifa ya Uchaguzi ndiyo inayogawa Majimbo.

Tatu, Manyoni Magharibi mpaka sasa ina watu wapatao 67,000, ina Vijiji 17, ina Kata 5 na Tarafa 1. Kwa hiyo, mpaka sasa hivi Manyoni haijakidhi vigezo ambavyo vimewekwa na Sheria ya Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba vigezo kwa Wilaya ya Manyoni Magharibi kuanzishwa bado havijafikiwa kabisa mpaka sasa hivi. *(Makofi)*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika swali lake la msingi Mheshimiwa Waziri, amezungumza kwamba idadi ya watu na ukubwa wa Wilaya ni kati ya vitu vinavyoangaliwa pamoja na vigezo vingine. Wilaya ya Geita sasa hivi ina watu wanaokaribia 800,000 ambayo inakaribia sawa na nchi ya Zanzibar na inakaribia karibu Mkoa wa Singida na kwa kuwa ukubwa wake unazidi baadhi ya Mikoa.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuifikiria zaidi kuwa Mkoa peke yake badala ya kufikiria kuigawa? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, mara ya mwisho kwenye Bunge lililopita tulitoa maelezo kuonyesha baadhi ya kazi iliyokuwa imefanyika katika kufanya tathmini ya maeneo ambayo yanaweza kugawanywa katika Wilaya mpya. Nilieleza kwamba tuna Wilaya 24 ambazo tulifikiria zinastahili ikiwemo Geita. Lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti Rais aliridhia Wilaya 8.

Kwa hiyo, kwa upande tuna hakika hali ikiruhusu pengine eneo hilo linaweza likagawanywa mara mbili. Lakini kwa vyovyote vile hauwezi kuwa ni Mkoa peke yake hata ingefanyika namna gani isingewezekana. Vigezo vyake bado havitafikiwa hata kidogo kwa sababu vigezo vinataka Mkoa ni angalau zaidi ya watu milioni moja. Sasa kama bado mko 700,000 sana sana labda Wilaya tukaikubali. *(Makofi)*

Na. 46

**Uhitaji wa Barabara Vijiji vya Jimbo la Kibakwe**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE** aliuliza:-

Kwa kuwa Vijiji vya Lufu, Mang'aliza, Mlimo, Matonya, Gwamuhungile, Galigali na Mbuga vipo milimani na vinakabiliwa na tatizo kubwa la barabara na kwa kuwa tangu tupate Uhuru hadi sasa Serikali zilizokuwa madarakani kwa awamu zote hazikuwahi kutengeneza barabara kwenye maeneo hayo, jambo lililosababisha hali ya usafiri kwenye maeneo hayo kuwa ya taabu sana, hata imefikia hatua ya kubeba wagonjwa kwenye machela na mizigo kubebwa na punda:-

Katika mazingira kama hayo, je, Serikali ya Awamu ya Nne inawaambia nini wananchi wa Vijiji hivyo?

**NAIBU WAZIRI , OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, naomba kutoa maelezo mafupi kuhusu jiografia ya Vijiji alivyovitaja kama ifuatavyo:-

Barabara ya Chang'ombe - Mlimo - Lufu hadi Gwamuhungile na ile ya Ikuyu - Makang'aliza ni barabara za Vijiji na pia barabara ya Lumuma - Mbuga - Galigali hadi Matonya ni barabara ya Wilaya *(District roads).* Hivyo barabara ya Lumuma - Mbuga inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa na barabara za Chang'ombe - Gwamuhungile na Ikuyu - Makang'aliza zinahudumiwa na Vijiji husika. Barabara hizi zipo katika safu za milima mikali inayopelekea kazi ya kusafirisha mitambo mikubwa ya kutengeneza barabara katika baadhi ya maeneo haya kuwa ngumu.

Si kweli kwamba tangu tupate Uhuru hadi sasa Serikali zilizokuwa madarakani zote tatu hazikuwahi kutengeneza barabara hizo, kwani Serikali zote tatu zimechukua

hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa barabara za Wilaya zinapitika na zinatengenezwa kwa kutumia fedha za mfuko wa barabara *(road fund)* na kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya wananchi wamehamasishwa kutengeneza barabara za Vijiji ili kuwapa fursa ya kutoa mchango wao katika shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshiriki katika matengenezo ya barabara kwenye maeneo hayo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 Serikali ilitoa jumla ya shilingi 26,472,000 kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Lumuma - Mbuga ambayo ni kilometa 23.

Pia katika mwaka 2004/2005 Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa katika kuunga mkono juhudi za wananchi katika matengenezo ya barabara hizo ilinunua vifaa mbalimbali vya matengenezo ya barabara hizo za Vijijini kama vile majembe, sululu, koleo, nyundo na kadhalika na kukabidhi kwa Serikali za Vijiji vya Mbuga, Galigali, Matonya na Kata ya Mbuga na Vijiji vya Nyandu, Matonya na Mwanawota katika Kata ya Wota kwa ajili ya matengenezo ya barabara hizo za Vijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2005/2006, Serikali imetenga jumla ya shilingi 8,220,000 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya kawaida kwa ajili ya barabara ya Lumuma - Mbuga na barabara Mbuga - Galigali. Kwa kufuata mpango wa matengenezo wa Halmashauri 2005/2006, zabuni zitatangazwa mwezi Aprili, 2006 kwa robo ya mwisho ya mwaka wa fedha.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa imeingia katika awamu ya pili ya utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* 2005/2006, mipango hiyo ya Halmashauri ni kuendelea kuhamasisha wananchi katika Vijiji hivi juu ya mbinu za kuibua miradi mbalimbali katika jamii kulingana na mahitaji yao, ikiwemo miradi ya matengenezo ya barabara za Vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne, inatambua umuhimu wa barabara za Vijiji hivyo kama kiungo muhimu cha uchumi wa wananchi wake na kwa kutambua hilo Serikali itaendelea kuzifanyia matengenezo barabara hizo kupitia fedha za Halmashauri pamoja na nguvu za wananchi kulingana na mipango ya matengenezo iliyopo ili kuondoa adha ya usafiri katika Vijiji hivyo. Hata katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2005 hadi 2010, Ibara ya 44 imeliweka wazi suala la mkazo wa matengenezo ya barabara Vijijini. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sababu hizo hizo za kuamini kwamba Halmashauri inaweza ikatengeneza barabara ndiyo iliyosababisha isiweze kutengemaa na kuweza kupitika na hata leo hii watu wanateseka kwa kupakia mizigo yao kwenye punda na kubeba wagonjwa kwenye machela na kwa kuwa wananchi wana imani kubwa na Serikali ya Awamu ya Nne, je, sasa Serikali haioni kuwa umefika wakati sasa ikabeba mzigo yenyewe wa kutengeneza barabara zile kwa sababu gharama yake ni kubwa na Halmashauri haiwezi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali langu la awali kwamba Serikali ya Awamu ya Nne, imetilia mkazo barabara za Vijijini na hata kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi hilo limeelezwa wazi. Pia mradi wa *TASAF* ambao kila Wilaya watakuwa wamepewa shilingi bilioni moja na zaidi kwa ajili ya miradi ya Vijiji mbalimbali. Ningeshauri Mbunge pamoja na Halmashauri yake wangeweka mkakati wa kuweza kutengeneza barabara hii kwa kutumia hela za *TASAF* kwa sababu ni Vijiji vyenyewe ambavyo vinatakiwa kuibua miradi ambayo wanaona kwamba ni kero katika Vijiji vyao. *(Makofi)*

Na. 47

**Tatizo la Ombaomba Mijini**

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALIFAN** aliuliza:-

Kwa kuwa tatizo la ombaomba halijengi taswira nzuri kwa Taifa letu na kwa kuwa wimbi hilo si tu linawahusisha wazee wenye umri mkubwa bali hata watoto wenye umri wa kwenda shule wameingia katika shida hiyo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani kabambe wa kudhibiti hali hiyo isiendelee?

(b) Je, iko sheria inayowalinda vijana wenye umri wa kwenda shule wasiendelee na biashara hiyo ya ombaomba?

**NAIBU WAZIRI , OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Mbunge wa Tumbe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuwepo kwa ombaomba Mijini hakujengi taswira nzuri kwa Taifa letu, hasa inapowahusisha watoto wenye umri wa kwenda shule. Katika kukabiliana na tatizo hilo, Serikali imechukua hatua mbalimbali kuhakikisha kwamba watoto wenye umri wa kwenda shule wanapata fursa ya kwenda shule. Hatua hizo ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Kutunga na kutekeleza sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 inayotaka kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule aende shule.

(ii) Kuandaa na kutekeleza mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi *(MMEM)* ili kuwezesha kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule aende shule.

(iii) Kutekeleza kwa majaribio *(on a pilot basis)* Mpango wa Elimu ya Msingi kwa walioikosa *(MEMKWA)* ili hata watoto waliovuka umri wa kuhudhuria elimu ya kawaida ya msingi waweze kupatiwa elimu hiyo.

(iv) Serikali imeandaa na inaanza kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari *(MMES)* ili watoto watakaofaulu mitihani ya kumaliza elimu ya msingi waendelee na elimu ya sekondari na hatimaye elimu ya juu. Pia Serikali kupitia Halmashauri inatoa ruzuku kwa kuwasomesha watoto wanaotoka kwenye familia duni wakiwemo watoto wa mtaani na ombaomba.

(v) Pia Serikali kupitia viongozi wakuu imekuwa ikihimiza na kuhamasisha upanuzi wa shule, mafunzo na ajira ya walimu na kutenga maeneo kwa ajili ya sekta binafsi kushiriki katika utoaji wa elimu msingi.

Aidha, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005/2010 imezungumzia mikakati mbalimbali ya kuyaendeleza makundi maalum. Makundi hayo ni pamoja na watoto, wanawake, vijana, wazee, walemavu na kadhalika. Makundi hayo yameshaanza kuwezeshwa kwa kupewa mikopo ili kujikimu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ustawi kwa Jamii kwa kushirikiana na Halmashauri nchini imekuwa ikifanya juhudi za kuwatafuta jamaa na wazazi wa watoto ombaomba na kuwarudisha kwenye familia zao. Pia imeanzisha makazi ya wasiojiweza na kukosa hifadhi toka kwa jamii ili wahudumiwe na Serikali. Juhudi zingine ni pamoja na ufunguaji wa vyuo vilivyopo chini ya Mamlaka ya Ufundi Stadi nchini *(VETA)*. Aidha, sekta binafsi pia hujihusisha katika kudhibiti watoto kuwa ombaomba kwa kuanzisha vyama visivyo vya Kiserikali *(NGO)* na asasi mbalimbali za kuwalea watoto yatima na waishio katika mazingira magumu.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu (a) hapo juu sheria inayowalinda vijana wenye umri wa kwenda shule wasiendelee kuwa omba omba ipo nayo ni sheria Na. 25 ya mwaka 1978. Naomba nitumie fursa hii kuzihimiza Halmashauri zote nchini kuitumia kwa ukamilifu sheria hiyo ili kuhakikisha kwamba watoto wenye umri wa kwenda shule hawawi ombaomba bali wanahudhuria elimu ya msingi. Aidha, pale inapobidi, Halmashauri zitunge na kutekeleza sheria ndogo ndogo ili kuhakikisha kwamba watoto wote wanaandikishwa na wanahudhuria elimu ya msingi.

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sheria ya kuwalinda watoto wadogo ipo na kwa kuwa bado wimbi hilo la watoto wadogo na hasa kushirikishwa ndani ya biashara ya ombaomba na wazazi wao inaendelea je, Serikali ipo tayari sasa kuwachukulia hatua wazazi ambao wanawashirikisha watoto wao moja kwa moja katika biashara ya ombaomba? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Serikali za Vijiji zimepatiwa *register* na hizo *register* zinaweka idadi ya wakazi wote wanaoingia na wanaotoka katika sehemu mbalimbali. Kwa hiyo, Sheria hii hizo *register* zinawabana watu wasiwe

wanakwenda sehemu nyingi au wasiwe wazururaji kwa sababu *register* iko katika kila kijiji. Mgeni yeyote anapoingia kwenye mtaa au kwenye kijiji, Serikali ya Kijiji au Serikali ya Mtaa lazima itambue hilo. Kwa hiyo, Serikali, inabana watu wasizurure au wasiwe ombaomba kwa kutumia *register* za Vijiji au *register* za Mitaa.

Kwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa hilo wanalitambua na kwa Wenyeviti wa Vijiji hilo wanalitambua ni jukumu mojawapo la hao Wenyeviti wa Vijiji na wa Mitaa katika kuhakikisha kwamba watu hawaingii ovyo katika Mitaa na hawatoki ovyo katika Mitaa. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mimi ninajua hakuna mtoto yeyote anayeitwa mtoto wa mtaani na Mheshimiwa Waziri ameziagiza Halmashauri za Manispaa na za Wilaya kuhakikisha kwamba watoto saa za kazi wanakwenda shuleni na kwa kuonyesha mfano ukitoka nje hapo utaona watoto wengi wanaosha magari pale. Je, Serikali inasema nini kukemea jambo hili? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, jukumu hili la kuhakikisha hatuwi na watoto ombaomba wakati mwingine tunaweza tukadhani ni Serikali, lakini ni letu wote kila mzazi kwa nafasi yake anapaswa kutambua hilo na kila Mtanzania anapaswa kuliona hilo. Kwa hiyo, kiutaratibu tutaendelea kutumia sheria, lakini mimi nadhani kwa sehemu kubwa jamii ndiyo tunapaswa ku-*take responsibility* katika kujaribu kuhakikisha jambo hili haliendelei kama inavyoonekana hivi sasa. *(Makofi)*

Na. 48

**Tatizo la Ajira kwa Vijana**

**MHE. HAZARA P. CHANA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi katika Sera ya Vijana kuna ahadi ya kuongeza ajira ya vijana.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha *Job Centres* ili vijana waweze kupata ajira kwa urahisi?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani katika kutimiza suala la ajira kwa vijana?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hazara Pindi Chana, Viti Maalum, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua wazi kuwa miongoni mwa changamoto kubwa tuliyonayo ni pamoja na suala zima la ukosefu wa ajira hasa kwa vijana. Tunazungumzia ajira, tunazumgumzia ajira za kujiajiri *(Informal Sector)* na ajira za kuajiriwa katika *formal sector.*

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine inaandaa mkakati wa kujenga mazingira mazuri ya kukuza sekta isiyo rasmi kama mwajiri mkubwa wa vijana. Aidha, Serikali inaendelea kuboresha miundombinu, utaalamu, mitaji na nyenzo za kuwawezesha vijana kufanya kazi zenye tija na kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hazara Pindi Chana, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Hivi sasa Serikali ina kituo kimoja cha Ajira *(Labour Exchange Centre)* ambacho kipo Dar es Salaam. Kituo hiki kilianzishwa mwaka 2001 ili kukidhi mahitaji ya ajira kwa vijana kwa kuwasaidia wale wanaotafuta kazi kwa kuwaunganisha na waajiri na pia kuwasaidia wale wanaotaka kubadili aina ya kazi wanayoifanya wapate kazi wanayoihitaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uzoefu uliopatikana, Wizara yangu inakusudia kuongeza vituo vingine katika majiji ya Mwanza, Arusha na Mbeya na hatimaye kama Bajeti itakavyokuwa inaruhusu kufungua vituo katika mikoa hatua kwa hatua. Kwa mwaka wa fedha ujao 2006/2007 tunakusudia kufungua kituo cha Mwanza kuendelea na maandalizi katika vituo vingine.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kutambua kuwa suala la ajira kwa vijana ni suala mtambuka *(cross cutting)* hivi sasa inaboresha mikakati ya zamani na kuandaa mkakati wa kitaifa wa kukuza ajira *(National Employment Creation Strategy)* ambao utawahusisha wadau wote.

Mheshimiwa Spika, mikakati hiyo ni pamoja na kushirikiana na sekta zinazohusika kuboresha mazingira ya mijini na vijijini kwa kuyafanya yawe ya kuvutia na yenye kuwapatia vijana ajira pale waliko, kuwahamasisha vijana kupenda na kushiriki katika kilimo, kuweka mfumo mzuri wa utoaji mikopo na huduma nyingine za kibenki kwa vijana na kuwahamasisha vijana kuanzisha vyama vya akiba na mikopo *(SACCOS).*

Aidha, Wizara inahimiza kuwa vijana katika kila Tarafa zinazolingana na soko la ajira, kutoa mafunzo ya stadi mbalimbali na programu za ajira zinazolingana na soko la ajira, kuimarisha programu zitakazowasaidia vijana kupata fursa za kufanya kazi kwa vitendo *(on job training)* ili kuongeza ujuzi wao, kuwapa vijana mafunzo ya kuwawezesha kuajiriwa *(Ehancement of skills)* na kuongeza mtaji na wachangiaji wa mfuko wa vijana na kuviwezesha vyama vya *SACCOS* vya vijana kukopeshwa moja kwa moja kutoka kwenye mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote ambao ni wadau wa azma hii ya Serikali ya kuwapatia vijana ajira kuwa

tushirikiane kwa pamoja katika kuwapatia vijana fursa mbalimbali za ajira, hususan kuwahamasisha vijana kwa kuunda vikundi vya uzalishaji mali na kuanzisha *SACCOS* kwa kuwakopesha mikopo ili kupanua na kuongeza ubora wa bidhaa wanazozizalisha.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Hazara Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum, kwa dhati yake ya kuwajali vijana katika nchi yetu. *(Makofi)*

**MHE. HAZARA P. CHANA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Pamoja na majibu mazuri kwa kutambua kuwa *population* ya Mkoa wa Iringa zaidi ya asilimia 70 ni vijana.

Je, Serikali na Wizara itakubaliana nami kwamba katika Mikoa ambayo wanatarajia kufungua hizo *labour access center* Mkoa wa Iringa upewe kipaumbele?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO):** Mheshimiwa Spika, katika swali langu la msingi nimesema kwamba tutaanza na Mwanza, Arusha na Mbeya. Hii ipo katika programu yetu. Lakini pia tumesema tutaendelea katika Mikoa yote hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, ni kwa mantiki hiyo hiyo na Mkoa wa Iringa utakuwa katika mkakati huo wa hatua kwa hatua kwa Mikoa yote. *(Makofi)*

Na. 49

**Ajira ya Kudumu**

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI** aliuliza:-

Kwa kuwa ukosefu wa ajira ni tatizo kubwa hapa nchini na kwa kuwa kuna viwanda ambavyo huwatumikisha watu zaidi ya miaka mitatu pasipo kuwaajiri hali ambayo husababisha watu wengi kupoteza ajira wakati wowote:-

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha Sheria ya Kazi inafuatwa ili wapate ajira za kudumu muda unapofika?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inapitia katika mabadiliko makubwa ya kijamii, kisiasa na kiuchumi, hali ambayo imefanya sheria, kanuni na taratibu za kupanga na kutekeleza mipango yetu kubadilika sana. Vivyo hivyo, sheria za kazi zilizopo pia zimekuwa na upungufu katika utekelezaji wake, usiozingatia mahitaji yaliyopo sasa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu huo Septemba, 2001 Waziri wa Kazi wakati huo aliunda Tume maalumu *(Task Force)* iliyoongozwa na Jaji John Mrosso wa Mahakama ya Rufaa kuzitayarisha upya sheria za kazi ili kurekebisha kasoro zilizokuwepo. Sheria mpya zimeainisha maeneo mbalimbali yenye kuzingatia haki na maslahi ya wafanyakazi na waajiri wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mwaka 2004 Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria Na. 6 ya Ajira na Mahusiano Kazini ambayo imezingatia haki na maslahi ya wafanyakazi na waajiri. Kifungu cha 14 cha Sheria hiyo kimeweka bayana aina tatu za mikataba:-

1. Mkataba ambao hauna muda maalum *(unspecified contract);*

2. Mkataba wa muda maalum kwa watu wa menejimenti na watu wenye taaluma maalum *(Professionals and Managerial Cadre);* na

3. Mkataba kwa ajili ya kazi maalum *(Contract for a specific task).*

Mheshimiwa Spika, kutokana na mikataba hiyo, ni dhahiri kwamba mtu akipata ajira atakuwa katika moja ya makundi haya. Hivyo Sheria mpya itakapoanza kutumika hali ya ukibarua nayo itakoma.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa matakwa ya sheria yanatekelezwa, Wizara yangu itaimarisha ukaguzi katika maeneo ya kazi *(Labour Inspection).* Aidha, taratibu za kukamilisha maandalizi ya utekelezaji wa Sheria Na. 6 ya mwaka 2004 ili ianze kutumika na kuondoa adha wanayopata Wafanyakazi, zinaendelea hivi sasa. Tunatarajia kanuni hizi zitakuwa tayari tarehe 1 Agosti, 2006.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Lakini kwa ruksa yako sasa naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa ambazo zimefanyika na Serikali kwa maana ya kuwalipa mafao wale watumishi wa viwandani waliostaafishwa baada ya vile viwanda kuwa vimebinafsishwa. Lakini bado wale wanaolipwa hawajui kiasi halisi ya fedha ambacho wanapashwa kulipwa.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile wanalipwa kwa karatasi wanasaini kwenye karatasi badala ya kusaini vocha kwa maana hiyo hawabaki na ile *copy* inayoonyesha fedha walizolipwa. Je, Serikali itadhibiti vipi malipo hayo kuhakikisha kwamba fedha zote zilizopelekwa kule wameweza kulipwa wale watumishi?

La pili ambalo ningehitaji kujua ni kile kiwango cha ujira wa vibarua kwamba hivi kila kibarua kiwango cha chini anachopashwa kulipwa ni kiasi gani na haya malipo ya vibarua yanalipwa, ni kwa wale wa viwandani peke yake au ni kwa vibarua wote hata wale wanaofanya kazi za nyumbani? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO):** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kwamba mafao ya watumishi wa vilivyokuwa viwanda vya umma wanalipwa. Lakini kwa sababu suala hili linaonekana ni suala *specific* ingekuwa vizuri kama Mheshimiwa Vedastus Manyinyi angetuona rasmi akatupa zile *detail* ili tuweze kulifanyia kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni la jumla mno ili tuweze kumpa majibu ambayo yanaridhisha tuweze kujua ni wa kiwanda kipi, shirika lipi, katika maeneo ambayo anayazungumzia Mheshimiwa Vedastus Manyinyi. Kwa hiyo, ningeshauri baadaye tuonane atupe hizo *details.*

La pili, ni kiwango cha chini cha vibarua, kama tulivyosema kwenye swali la msingi tuko katika soko huria na mikataba ya kazi ina *vary* kutoka mwajiri mmoja hadi mwajiri mwingine. Lakini hata hivyo kiwango cha chini cha mshahara cha nchi yetu inafahamika ni shilingi 58,000 kwa viwango vya Serikali. Lakini hivyo waajiri hao wamekuwa wakiingia mikataba na waajiriwa kwa maelewano kulingana na mikataba ile. Kwa hiyo, nalo hili Mheshimiwa Vedastus Manyinyi kama kuna jambo *specific* tunaweza tukalijadili vizuri ili tukupe majibu ambayo ni muafaka kabisa.

Na. 50

**Jinsi ya Kupata Uwiano wa Wabunge Wanawake Bungeni**

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa upo utaratibu wa kuwapata Wabunge Wanawake Bungeni kwa kupitia uwakilishi wa Majimbo. Uteuzi wa uwiano wa vyama, Baraza la Uwakilishi na uteuzi wa Mheshimiwa Rais unabainisha kwamba uwiano wa Wabunge Wanawake na Wabunge wanaume unaweza kuboreshwa kufikia uwiano wa 50% ifikapo mwaka 2010:-

Je, Serikali itakubali iundwe Kamati ya Bunge kuandaa mapendekezo ya namna ya kutekeleza azma hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba azma ya Serikali ni kuongeza uwiano wa idadi ya Wabunge Wanawake Bungeni. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali imechukua hatua mbalimbali katika kuhakikisha kuwa idadi ya Wabunge Wanawake inaongezeka

kufikia kiwango chake ilichojiwekea na kile kilichowekwa na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika pamoja na kile kilichowekwa na Azimio la Umoja wa Afrika *(AU)* la mwaka 2004.

Hatua hizo ni pamoja na kuwasilisha Miswada miwili ya Sheria ya Mabadiliko ya Kumi na Tatu na Sheria ya Mabadiliko ya Kumi na Nne ya Katiba ya Nchi. Bunge lilipotunga Sheria hizo, liliwezesha kuwepo kwa Wabunge wa Viti Maalumu kwa utaratibu wa uwiano wa Wabunge. Ibara za Katiba zilizofanyiwa mabadiliko ni Ibara ya 66 (1) (b) na 78.

Mheshimiwa Spika, kadhalika, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inatumia kila fursa inayopatikana katika kuwahamasisha wanawake kujitokeza na kushiriki chaguzi katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, Serikali inatumia uwezo wake wa hali na mali kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya vyama vya kiraia, asasi zisizo za kiserikali, mashirika ya dini na kadhalika ambayo yanashiriki kuelimisha na kuhamasisha wanawake kujitokeza katika kugombea nafasi za Ubunge, Udiwani na nafasi nyinginezo za kisiasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina imani kuwa kwa kuzingatia juhudi kubwa inayofanya na juhudi zinazofanywa na vyama vya kiraia, asasi zisizo za Kiserikali, mashirika ya kidini pamoja na wadau mbalimbali katika kuhamasisha wanawake kushiriki katika uongozi na hatua kubwa tuliyofikia hivi sasa haioni sababu ya kuunda Kamati Maalum ya Bunge kwa ajli ya kuandaa mapendekezo ya kutekeleza azma hii.

Na. 51

**Athari za Kuahirisha Uchaguzi Mkuu 2005**

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa kifo cha mgombea mwenza wa nafasi ya Urais kwa chama kimojawapo kiliathiri utaratibu mzima wa suala la uchaguzi wa mwaka 2005 na kuwafanya wagombea pamoja na vyama vyao kupata adha kubwa sana kugharimia awamu mpya ya kampeni zao kwa sababu Bajeti zao za awali zililenga tarehe 30 Oktoba, 2005 na sio tarehe 14 Desemba, 2005 na kwa kuwa kutokana na hali hiyo ilibidi tarehe ya Uchaguzi Mkuu iliyopangwa hapo awali iahirishwe hadi tarehe 14 Desemba, 2005:-

(a) Je, Serikali ina msimamo gani kuhusu suala hilo?

(b) Je, Serikali itachukua hatua gani ili kuepuka tatizo kama hilo kwa siku za baadaye?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma, Mbunge wa Kalenga, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kutokana na kuahirishwa kwa Uchaguzi Mkuu toka Oktoba 30, 2005 hadi Desemba 14, 2005 gharama za uchaguzi ziliongezeka kibajeti kutokana na kampeni hizo kuanza upya. Hivyo, kwa niabaya Serikali napenda kwanza kuwapa pole wagombea wote kwa uvumilivu wao kwa kipindi chote cha kampeni na uchaguzi na hususan kwa kuingia gharama za ziada zilizosababishwa na kuahirishwa huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya kuangalia upya Sheria katika eneo hili.Uzoefu katika uchaguzi uliopita umeonyesha kwamba uchaguzi unapoahirishwa kwa muda mrefu na kampeni kuanza upya, kunakuwa na gharama za ziada na vile vile wapiga kura pamoja na wagombea wanachoka.

Mheshimiwa Spika, kila baada ya Uchaguzi Mkuu, Tume ya Taifa ya Uchaguzi hutoa tathmini kuhusu Uchaguzi Mkuu. Serikali itaitafakari tathmini ya Tume kuhusu Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 na vile vile itafanya kila jitihada kubaini matatizo yoyote yaliyojitokeza katika Uchaguzi uliopita. Nia ya Serikali ni kuleta mapendekezo ya kurekebisha upungufu wowote utakaobainika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati akijibu swali Na. 4 tarehe 28 Machi, 2006, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Philip Marmo alilieleza Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inakusudia kuanzisha mjadala wa Kitaifa ambao utawahusisha wadau wote vikiwemo vyama vya siasa ili kupata mustakabali kuhusu marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi kwa jumla ambapo suala hili na mengineyo yatawekwa wazi. Maamuzi yatakayofikiwa katika mjadala huo yatakuwa ni sehemu ya vipengele vitakavyoingiza kwenye marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pili namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo ni mazuri na yanaridhisha. Lakini pamoja na hayo ningependa kuuliza swali moja. Je, Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba kwa sababu ya athari kubwa ambazo Wizara inakubali, iko haja ya kuharakisha zoezi hilo alilolizungumzia?

Pili, nitoe ushauri kidogo kwamba muda utakapofika kwa waandishi wa sheria *(Draftmen),* utumike umakini mkubwa sana. Watazame mbali, watazame makando kando na mambo yote yanayoweza kutokea *inventualities* kwa sababu tatizo hili limetokea kutokana na kutokutazama mbali. Je, Waziri atakubaliana nami katika ushauri huo?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nataka nimweleze kwamba zoezi hili la kuanzisha mjadala wa Kitaifa liko katika hatua za mwisho za maandalizi na semina za mwanzo mwanzo zitaanza mwisho wa mwezi Mei. Hivyo nafikiri ni haraka vya kutosha. *(Makofi)*

Pili, napenda nikubaliane na ushauri wake kwamba tutakapokuwa tunaziandika tena Sheria hizi ambazo zitakuwa zinapendekezwa basi tutaangalia mbali na tutazingatia ushauri wake. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Anna Komu aliipata nafasi hiyo ya Ugombea Mwenza kwa mujibu wa Katiba ilivyo hivi sasa, kwa kufuata taratibu zote ambazo zilikuwepo. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami achukue ushauri wangu katika huo mjadala kila mgombea mwenza awe ana *reserve* wake yaani mtu wa akiba? *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, tunasema tunaanzisha mjadala wa Kitaifa. Tunategemea kama hayo nayo yatapita katika mjadala huo basi yatakuwemo kwenye sheria.

**SPIKA:** Nadhani ni haki kwamba niwape na CHADEMA waulize nyongeza. Kwa sababu wanahusika.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuonyesha haki hiyo na nina swali la nyongeza ambalo lina vipengele vitatu:-

(a) Mgombea Mwenza aliyefariki ni wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Marehemu Mzee Jumbe Rajab Jumbe na wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu swali la msingi ametoa pole kwa wagombea kwa kupata taabu . Hajatoa pole kwa chama kilichofiwa. Sasa je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza sasa akatoa pole kwa CHADEMA kwa kufiwa na Mgombea Mwenza wake? *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa kwa swali la msingi. *(Makofi)*

Sasa naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kabwe Zitto kuwa mgombea mwenza wa CHADEMA alipofariki Watanzania wote waliondokewa na Mtanzania mwenzao. Kwa hiyo, nawapata Watanzania wote pole. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nawapa wana CHADEMA pole na ningependa kuungana mkono na Naibu Waziri kuwapa pole Wabunge wote kwa subira waliyokuwa nayo na kwa gharama iliyoongezeka na kwa Serikali. *(Makofi)*

Na. 52

**Tatizo la Ugonjwa wa Kansa Nchini**

**MHE. NURU A. BAFADHILI (k.n.y. MHE. RIZIKI OMAR JUMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Watanzania wengi hivi sasa wameathirika zaidi na ugonjwa wa kansa za aina mbalimbali, maradhi ambayo katika miaka ya nyuma yalikuwa adimu sana:-

(a) Je, Serikali kupitia Wizara ya Afya inaweza kuliambia Bunge kwamba ni utafiti gani umefanywa kutafuta chanzo cha ugonjwa huo na sababu za kuongezeka kwa kasi siku hadi siku?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa muda mrefu wa kupunguza kasi ya ongezeko la ugonjwa huo badala ya kusubiri kutibu?

(c) Je, ni sehemu gani ya nchi yetu ambayo imeathirika zaidi na ugonjwa huo hatari?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Kwanza napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba kansa inaitwa saratani kwa Kiswahili sanifu. Neno hili linalojumuisha magonjwa tofauti zaidi ya mia moja na sio ugonjwa mmoja kama wananchi wengi wanavyodhani. Hii inamaanisha kwamba magonjwa haya ambayo kwa ujumla wake tunayaita saratani yana vyanzo tofauti, dalili tofauti na yanahitaji mikakati tofauti kuyadhibiti.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utafiti mwingi umefanywa kutafuta chanzo na hapa naweza nikaorodhesha baadhi ya matokeo ambayo tunayo:-

(i) Saratani ya shingo ya kizazi yaani *uterus,* chanzo kikubwa ni *Human Papilloma Virus.*

(ii) Saratani ya mapafu, chanzo kikuu ni tumbaku na uvutaji wa sigara.

(iii) Saratani ya ini, chanzo ni kirusi aina ya *Hepatitis B.*

(iv) Saratani ya tezi na *Kaposi's Sarcoma,* chanzo ni kirusi aina ya *HIV.*

(v) Saratani ya *Burkitt's Lymphoma,* chanzo ni kirusi aina *Ebstein Barr Virus (EBV).*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile umefanyika utafiti za kemikali na vyakula vinavyosababisha saratani nchini. Hii imedhihirisha kwamba theluthi moja ya saratani inasababishwa na vyakula tunavyokula. Kwa mfano kemikali inaitwa *Aflotoxin*

inayopatikana katika karanga ambazo hazikuhifadhiwa vizuri na hatimaye zikaota ukungu, zinaweza kuleta saratani ya ini.

Mheshimiwa Spika, katika jibu langu nimesema hivi ni vyanzo vikuu na siyo vyanzo pekee. Utaona wagonjwa wengi wenye UKIMWI hawajapata kansa kutokana na tafiti nilizovitaja.

Mheshimiwa Spika, ieleweke basi kwamba vyanzo hivyo nivilivyotajwa vinasababisha saratani kwa kushirikiana na mambo mengine katika mazingira yanayomzunguka mwananchi, vile vile tofauti za kimaumbile *(genetic composition)* zinachangia. Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la saratani nchini kutokana na ongezeko la umri wanaoishi Watanzania. Saratani inawaandama zaidi watu wenye umri mkubwa. Lakini vile vile kumekuwa na ongezeko la uvutaji wa sigara, ugonjwa wa UKIMWI na utumiaji wa vyakula vilivyohifadhiwa kwa kutumia Kemikali mbalimbali.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ikishirikiana na Shirika la Afya Ulimwenguni inaandaa mpango wa Kitaifa wa kudhibiti saratani. Mpango huo pamoja na matibabu utatoa kipaumbele kwa kutoa elimu ya kuzuia saratani na kutoa huduma ya uchunguzi inayolenga kugundua chembechembe ambazo zinaonyesha uwezekano wa kubadilika kuwa saratani yaani *screening.* Hadi sasa huduma hii inapatikana kwa saratai za shingo ya kizazi na matiti. Ningependa nitumie muda huu kuwashukuru Chama cha Wanawake Madaktari Tanzania yaani *MEWATA* kwa kazi nzuri sana wanayofanya katika kupambana na Saratani ya Matiti. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, katika kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kuhusu ni sehemu gani ya nchi yetu ambayo imeathirika zaidi na ugonjwa wa saratani, ninapenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa vile ni asilimia ishirini tu ya wagonjwa wanaokisiwa kuwa na ugonjwa huu ndiyo wanafika na kutibiwa katika hospitali zetu, takwimu tulizonazo inawezekana hazionyeshi hali halisi ya tatizo la saratani katika jamii ya Watanzania. Kwa mfano takwimu kutoka taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* kuanzia mwaka 1982 mpaka 1997 zinaonyesha kwamba mkoa wa Dar es Salaam ukifuatiwa na mikoa ya Morogoro, Kilimanjaro, Mbeya, Tanga na Mwanza ndio inayoongoza kwa idadi ya wagonjwa waliotibiwa. Inawezekana kwamba mikoa hii imeleta idadi kubwa ya wagonjwa kutokana na urahisi wa kusafiri kufuata matibabu *Ocean Road Hospital* ama upatikanaji wa huduma za rufaa katika maeneo wanayoishi.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, hapa nchini yapo matibabu zaidi yanayoweza kupatikana dhidi ya ugonjwa huu zaidi ya matibabu yanayopatikana kutokana na mionzi ambayo inachomwa katika Hospitali ya *Ocean Road* na hatimaye inakuwa ni vifo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, magonjwa ya saratani kuna namna nyingi tunaweza kuyatibu. Moja ni kwamba kama kuna uvimbe ukiwa unaweza ukautoa kwa oparesheni. Kuna wengine tunatumia dawa, tunaita *thymotherapy* na wengine tunawamulika kwa mionzi. Aina hii ya matibabu ndiyo

inayopatikana kila mahali duniani. Sasa sielewi anaposema kwamba hii mionzi ndiyo inawafanya watu wafe, nadhani si sahihi. Tunatoa ili watu wapone na kama watakufa kwa kawaida wanakufa kwa sababu ya ugonjwa wa saratani walionao.

Na. 53

**Mkakati wa kuwa na Dawa za kutosha Nchini**

**MHE. MARIAM R. KASEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina jukumu la kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha madawa ya kutosha yanakuwepo katika hospitali na zahanati ili kuondoa adha iliyopo ya wagonjwa kuandikiwa dawa ambazo hazipo na kuwashauri wanunue dawa kwenye maduka binafsi?

(b) Je, haioni kuwa wananchi wanahatarisha afya zao kwa kununua dawa bila kupata vipimo na kwamba wanaweza kuuziwa dawa tofauti na ugonjwa unaohusika?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika juhudi za Serikali kuhakikisha upatikanaji wa dawa katika zahanati, vituo vya afya na hospitali, Serikali imekuwa ikiongeza Bajeti ya dawa mwaka hadi mwaka. Katika kipindi cha miaka mitatu, Bajeti ya dawa na vifaa ilikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Mwaka wa fedha 2003/2004 Serikali ilitenga shilingi 25,000,000,000.

(ii) Mwaka wa fedha 2004/2005 zilitengwa shilingi 35,175,356,000.

(iii) Mwaka wa fedha tulionao zimetengwa shilingi 47,394,729,600.

Mheshimiwa Spika, ongezeko hilo la Bajeti limeboresha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika zahanati, vituo vya afya na hospitali.

Pamoja na Bajeti ya Serikali kuongezeka mwaka hadi mwaka, pia vituo vyetu vya kutolea huduma za afya (zahanati, vituo vya afya na hospitali) vinakusanya fedha kutokana na vyanzo mbalimbali vya uchangiaji wa huduma za afya, kama mnavyojua tuna mifuko mbalimbali, kama Mfuko wa Afya ya Jami, Mfuko wa Bima ya Afya na *cost sharing.* Fedha zinazopatikana hutumika kununua dawa na kuziba upungufu unapojitokeza. Tatizo kubwa sio upungufu au uhaba wa dawa bali ni usimamizi mbovu wa dawa zilizopo. Halmashauri zimeelekezwa kuunda Bodi za Afya na mahali ambapo

Bodi hizo ni makini na zinasimamia vizuri shughuli za afya upatikanaji wa dawa na huduma mbalimbali za afya umeboreshwa.

Napenda nitumie fursa hii kutoa wito kwenu Waheshimiwa Wabunge pamoja na Madiwani kuwa makini na Bodi za Afya tuzisimamie ili kuwapunguzia wananchi kero mbalimbali za huduma za afya. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ni muhimu ugonjwa ukatambulika ili mgonjwa apewe dawa sahihi. Vipimo vinasaidia kufikia utambuzi wa ugonjwa *(diagnosis)* lakini kuna maradhi ambayo yanaweza kutambulika bila vipimo. Wananchi wanahatarisha afya zao kwa kutumia dawa ovyo bila maelekezo ya mganga au daktari. Hivyo, wananchi wanashauriwa kupata dawa toka katika vituo vya kutolea huduma au kutoka maduka ya dawa ambayo yanayoendeshwa na mfamasia badala ya kujinunulia dawa kiholela. Dawa moto huuzwa katika maduka ya dawa kwa cheti cha daktari.

Naomba nitoe wito kwa wananchi kwamba dawa zimezagaa mitaani hasa Dar es Salaam na katika vituo vya mabasi zinauzwa kwenye mifuko ya *rambo* na nyingi zinatoka China. Ningeomba niwatahadharishe wananchi kwamba wanahatarisha afya zao kwa kutumia dawa ambazo hazijahakikiwa na Wizara yangu. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, wa Mkoa wa Mtwara hadi hivi sasa wako wengi ambao wanapata huduma za afya kwa zaidi ya umbali wa kilomita 10 na hatimaye kusababisha wakinamama wajawazito kujifungulia manjiani na hata kusababisha vifo:-

Je, Wizara haioni sasa ni wakati muafaka wa kuweza kuandaa mpango mkakati kama ilivyo *MMEM* au *MMES* kwa nchi nzima ili kutuwezesha kujenga Zahati za kutosha na kuweza kuondoa tatizo hili kwa jamii yetu ili kuwaletea Watanzania maisha bora na yenye afya bora?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri unaweza kujibu ingawa naliona ni swali tofauti kidogo, maana yake hili lilikuwa la dawa na hili la ujenzi wa Zahanati.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ombi la Mheshimiwa Mbunge ilikuwa kwamba tuwe na mkakati maalum kama vile wa *MMES* na *MMEM* na kama alikuwepo kwenye Semina tuliyokuwanayo kule Ubungo, hili ni suala nilizungumza wakati nazungumzia kwamba tunafanya mapitio ya sera ya afya ambayo inatuongoza mpaka sasa na ni mkakati ambao utakuwa mkubwa utahitaji pesa nyingi na ambao hautahusisha Mkoa wa Mtwara peke yake, lakini ni kwa nchi nzima.

**SPIKA:** Mheshimiwa Teddy Kasela-Bantu, upendeleo maalum, pole umetoka katika kuugua, swali la nyongeza.

**MHE. TEDDY L. KASELA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa, dawa zinazotoka Wizarani kupelekwa katika Wilaya zinakwenda bila mpangilio wa magonjwa yaliyo makubwa katika Wilaya hizo, kwa mfano, kwenye sehemu ya Malaria, dawa zinapelekwa nyingi za Kichocho badala ya kupelekwa dawa nyingi za Malaria:-

Je, Serikali ina utaratibu gani au mikakati gani kuhakikisha kwamba kwenye sehemu ya Malaria zipelekwe dawa nyingi na kwenye sehemu ya kichocho zipelekwe dawa nyingi za kichocho kupunguza upungufu wa watu kununua dawa kutoka kwenye Bima?

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa pole Mheshimiwa Kasella-Bantu kama wewe ulivyompa na pia nimjibu Mheshimiwa Kasella-Bantu kama ifuatavyo:-

Ni kweli Wizara yangu imeliona hilo, tumekuwa tukifungasha dawa zinazofanana kwa kila Kituo. Lakini tumegundua kwamba katika maeneo mengine, magonjwa hayapewi msisitizo kufuatana na mahali yalipo na vilevile dawa kuna *seasons* tofauti unaweza ukawa na Malaria nyingi wakati huu na unapata kiasi kilekile cha dawa za Malaria. Kwa hiyo, sasa hivi tumeanza kitu kinaitwa *indent system* ambacho wale wanaohusiaka katika vituo wanatueleza ni dawa gani zinahitajika kufuatana na magonjwa ambayo yanasumbua maeneo yale, lakini wasivuke kile kiwango cha pesa kinachohitajika kwa kila *Kit. (Makofi)*

Na. 54

**Ubia na Shirika la Ndege la Afrika Kusini**

**MHE. MOHAMED IBRAHIM SANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa ubia uliokuwepo baina ya Shirika la Ndege la Tanzania na la Afrika Kusini ulivunjika:-

(a) Je, ni kwa kiasi gani Zanzibar ilishirikishwa kikamilifu katika ubia huo uliovunjika?

(b) Shirika limepata hasara au faida gani muda wote tulioshirikiana na Shirika hilo la Afrika Kusini?

(c) Je, wapo Maofisa wangapi wanaowakilisha Shirika hilo kutoka Zanzibar katika Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti na ni wangapi wanaotoka Tanzania Bara?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza nieleze kwamba sio kweli kwamba ubia wa Serikali ya Tanzania na Shirika la Ndege la Afrika Kusini kuhusu *ATCL* ulivunjika. Ubia huo bado uko hai ingawa sasa umekumbwa na matatizo makubwa. Lakini kuhusu ushirikishwaji wa Zanzibar katika ubia huo ni kwamba ingawa Shirika Ndege la Tanzania lililobinafsishwa lilikuwa linatoa huduma Kisiwani Zanzibar, Shirika hilo halikuwa moja ya Taasisi za Muungano chini ya iliyokuwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

(b) Tangu kuanzishwa kwa ubia kati ya *ATCL* na Shirika la Ndege la Afrika ya Kusini, *ATCL* limepata hasara kama ifuatavyo:- Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, *ATCL* ilipata hasara ya Shilingi bilioni 8.7 na mwaka wa fedha 2004/2005, *ATCL* ilipata hasara ya Shilingi bilioni 9.3. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2005/2006 *ATCL* inatarajia kupata hasara ya Shilingi bilioni 6.7.

(c) Mheshimiwa Spika, kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya Ndege ya Tanzania yuko Mjumbe mmoja kutoka Zanzibar ambapo Wajumbe wanne wanatoka Tanzania Bara.

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Shirika hili limebaini hasara inayopatikana kwa kila mwaka na ni mzigo kwa Taifa, hivyo hawaoni umuhimu wa kuwa na mkakati maalum?

**WABUNGE FULANI:** Anasoma.

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa sisomi nilikuwa naangalia tu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Shirika hili limekuwa ni mzigo kwa Taifa kwani badala ya kuleta faida, linaleta hasara kila mwaka; Je, kuna mikakati gani ya lazima na ya haraka kulirejesha tena Shirika hili la Tanzania katika mikono ya Watanzania ambao wana uwezo wa kuliendesha na kufanya kazi kama lilivyokuwa likifanya mwanzo. Hatuoni kwamba Mikataba kama hii wakashirikishwa kikamilifu Wabunge?

**WABUNGE:** Unasaoma.

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Sisomi karatasi nyeupe. Hatuoni kwamba Mikataba kama hii wakashirikishwa Wabunge katika masuala ya kubinafsisha Mashirika ambayo ni moja katika vyanzo muhimu kwa Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, ubia kati ya Serikali ya Tanzania na Shirika la Ndege la Afrika Kusini umekumbwa na matatizo. Serikali imeamua kwamba ubia huo hauwezi kuendelea tena kwa sababu hauleti tija kwa Taifa. Lakini zipo taratibu za kisheria za kujikwamua na

taratibu hizo ndizo zinazoendelea sasa hivi na siwezi kusema ni lini zitakamilika. Kwa hiyo, tutajikwamua.

Lakini suala la kurejesha *Air Tanzania* kama ilivyokuwa, ningependa nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeamua kwamba bado kuna haja ya kuwa na Shirika la Ndege la Taifa, bado kuna haja. Kwa hiyo, wakati tunaendelea na taratibu za kisheria, kwa upande mwingine hatujafuta kabisa wazo la kuwa na Shirika la Ndege la Kitaifa, isipokuwa sikubaliani na Mheshimiwa Mbunge anaposema kwamba Wabunge washirikishwe katika jambo hili, katika mgawanyo wa kazi. Hii ni kazi ya Serikali, sio kazi ya Bunge. Kwa hiyo, naomba atuachie, Serikali itakapokuwa inafanya mambo haya itatoa taarifa kwa Wabunge na hivi sasa tunavyozungumza hata kesho nakutana na Kamati ya Miundombinu, kuieleza kwa undani zaidi tumefikia wapi katika suala zima hili la *ATC*.

Na. 55

**Ukosefu wa Nyumba za Mawaziri**

**MHE. GRACE S. KIWELU** aliuliza:-

Kwa kuwa, uuzaji wa nyumba za Serikali uliofanyika katika Serikali ya Awamu ya Tatu umesababisha Mawaziri wengi kukosa nyumba na kukaa hotelini:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kilichotumika kulipia gharama za Mawaziri hao katika hoteli hizo?

(b) Je, ni Mawaziri wangapi wameshapata nyumba na wangapi bado wapo hotelini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la msingi lenye vipengele (a) na (b) la Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kwanza nitoe ufafanuzi juu ya madai kuwa uuzaji wa nyumba uliofanywa katika Serikali ya Awamu ya Tatu umesababisha ukosefu wa nyumba kwa Waheshimiwa Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, napenda kutokubaliana na dhana hiyo kwa sababu hali ya makazi ya Viongozi, wakiwemo Waheshimiwa Mawaziri, kabla ya Serikali ya Awamu ya Tatu kufikia maamuzi sahihi ya kuuza nyumba kwa Watumishi wa umma, bado baadhi ya Mawaziri walikuwa hawakai kwenye nyumba za Serikali kwa vile zilikuwa hazitoshi. Wengi wetu mtakumbuka kuwa baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri walikuwa wakikaa kwenye nyumba za Mashirika ya Umma yaliyokuwa chini ya Wizara zao.

Baada ya kuanza utekelezaji wa maamuzi ya Serikali ya Awamu ya Tatu ya Baraza la Mawaziri ya kuuza na kujenga nyumba nyingine mpya, hivi sasa tuna nyumba za kutosha kwa Mawaziri wote wa Serikali ya Awamu ya hii ya Nne. Kwa maana

nyingine, maamuzi ya Serikali ya Awamu ya Tatu yametoa changamoto na kujenga misingi imara ya kuwa na nyumba za kutosha kwa Viongozi wengi wa Serikali na sio Waheshimiwa Mawaziri peke yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufafanuzi huu, naomba sasa nijibu swali la msingi la Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa vile kila Mheshimiwa Waziri aligharamiwa na Wizara yake, imetuwia vigumu kwa sasa kujua ni kiasi gani cha fedha kimetumika hadi taarifa toka Wizara mbalimbali zitakaporatibiwa na kuwekwa pamoja. Hata hivyo, tunafanya jitihada za kukusanya taarifa hii na pindi zitakapokuwa tayari tutaziwasilisha Ofisini kwako kujua gharama hizo za hoteli.

(b) Mheshimiwa Spika, Mawaziri wote 33 ambao hawakuwa wameuziwa nyumba, tayari wameshapewa nyumba za kuishi na Wakala wa Majengo *(TBA)* katika maeneo ya Masaki, Kijitonyama na Mikocheni na hivyo kutokuwepo na tatizo la makazi kwa Waheshimiwa Mawaziri.

**MHE. GRACE K. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri ambayo kidogo hayakunifurahisha, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Je, nyumba hizi zilizojengwa za Mawaziri watauziwa kama walivyouziwa ile awamu? Kma hawatauziwa, ni sababu zipi za msingi zinazotumika wasiuziwe?

(ii) Kwa kuwa, Serikali yetu inadai Makao Mkuu ya nchi yako Dodoma, kwa nini nyumba hizi hazikujengwa Dodoma?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, nyumba hizi zilizojengwa kama ambavyo ilitangazwa toka awali, ni nyumba ambazo ni *tide quarters* za Serikali na hazitauzwa. Ni dhamira ya Serikali kwamba baada ya kuuza zile nyumba ambazo zilikuwa chakavu na ni gharama kubwa kuzi-*maintain,* hizi nyumba kwa sababu ni mpya na zitaendelea kuwa katika himaya ya Serikali na zitaendelea kujengwa sio Dar es Salaam kwa ajili ya Viongozi wa Dar es Salaam tu, lakini katika Mikoa yote kwa Viongozi Wakuu na hata Wilayani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hizi nyumba haziuzwi, lakini kuhusu nyumba hizi kujengwa Dodoma kama tunavyojua, ni kweli kwamba azma ya Serikali ni kuhamia Dodoma. Lakini kwa sasa tunajua wote kwamba Mawaziri au Wizara nyingi bado ziko Dar es Salaam na Ofisi nyingi ziko Dar es Salaam na kwa hiyo, nyumba...

**WABUNGE:** Nyumba zipo.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Lakini pili kama Serikali itakuwa imehamia Dodoma tayari nyumba vilevile zimejengwa Dodoma na kwa hiyo, itakuwa ni suala la kupanga nani akae wapi.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwamba naomba nitumie nusu dakika kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake kwa kufanya kazi nzuri na vyema katika miezi 100. *(Kicheko)*

Najua ni siku, imeonekana kama vile miezi ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

Je, kwa kuwa kumekuwa na manung'uniko mengi sana juu ya uuzaji wa nyumba za Serikali ambayo ni pamoja na upendeleo na pia kwa kuwa pameoneka kwamba hakuna utaratibu wowote ambao ulifuatwa juu ya kuuza hizi nyumba za Serikali ambao ni pamoja na udhamini na kumwuliza au kupata kibali cha *CAG:-* Je, kwa kuwa ni Serikali ya Awamu ya Nne ambayo iko makini na inataka haki, iko tayari kutengeneza Tume itakayoweza kuchunguza utaratibu mzima wa mauzo ya *assets* za Serikali ambayo ni mali ya Wapigakura na ni mali ya walipakodi?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, suala la uuzaji wa nyumba sio suala ambalo limeanza katika Awamu ya Tatu. Nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili limeanza tangu mwaka 1961.

Nataka nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka 1963 paliundwa Tume ya Adu, mwaka 1975 paliundwa Tume ya Nsekela na mwaka 1983 paliundwa Tume ya Mramba ambazo zote zilizungumzia masuala ya nyumba.

Mheshimiwa Spika, katika suala la kuimarisha makazi katika miaka1962, 1969 na hadi 1975 zaidi ya nyumba 4,000 zilizokuwa za *National Housing* ziliuzwa kwa wananchi wa kawaida. Nyumba hizi ziko Ilala, ziko Sengerema, Mheshimiwa Cheyo anaweza akaenda akazicheki.

Lakini pia katika kutekeleza suala hili la makazi katika upande wa Watumishi wa Serikali, hadi sasa hivi jumla ya nyumba 8,000 zimeuzwa katika nchi nzima na suala hili linaendana na sheria, kuna walaka mbalimbali zimepitishwa lakini pia kupitia Sheria Na.30 ya mwaka 1997 iliyoanzisha *Executive Agency* na ambayo imepitishwa na kwenye Bunge hili.

Kwa hiyo, ni jukumu la Sera za Serikali na hasa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inasisitiza makazi kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, katika uuzaji wa nyumba hizi, hadi sasa hivi jumla ya nyumba 1,200 zimekwishajengwa katika nchi hii na katika bajeti ya mwaka huu 2006 kuna zaidi ya nyumba 600 zitajengwa.

Kwa hiyo, suala la kuuza, kujenga, kuuzwa, kujenga, litaendelea katika kuimarisha makazi ya wananchi. Lakini pia pataendelea kuwepo na baadhi ya nyumba ambazo zitaendelea kuwa *tide quarters* kwa ajili ya Watumishi wa Serikali. *(Makofi)*

Na. 56

**Wanafunzi Wanaoingia Vyuo Vikuu**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Historia inaonyesha kuwa Elimu ya Juu ni suala la Muungano:-

(a) Je, ni wanafunzi wangapi wamepata nafasi ya kuingia Vyuo Vikuu kuanzia mwaka 2003-2005?

(b) Je, kati ya hao ni wanafunzi wangapi wametoka Zanzibar kujiunga na Vyuo hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Elimu ya Juu ni moja ya masuala ya Muungano. Kwa mujibu wa takwimu za Elimu ya Juu, jumla ya wanafunzi 17,657 walijiunga na Vyuo Vikuu vya Umma kati ya mwaka 2003-2005.

(b) Mheshimiwa Spika, ni vigumu kutaja idadi ya wanafunzi kutoka Zanzibar waliojiunga na Vyuo Vikuu kwa vile vigezo vinavyotumika kudahili wanafunzi ni sifa za kitaaluma na sio eneo anakotoka.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya kumwuliza. Ni kweli kuwa sifa ndio zinazompeleka mwanafunzi katika Chuo. Lakini katika mazingira ya Watanzania hata majina tu unaweza kujua huyu anatoka wapi na huyu anatoka wapi. Sasa Serikali inaposema haiwezi kujua ni wanafunzi wangapi kutoka Zanzibar, naona hili ni kitu cha kutisha kidogo, sijui unasemaje?

Pamekuwa na hoja ya wanafunzi kukosa nafasi, sasa na wanafunzi wengi kutoka Zanzibar wanafanya vizuri lakini hawapati nafasi, sasa anaposema hawajulikani, sisi tuelewe vipi? Hebu atoe ufafanuzi kidogo.

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri katika swali msingi.

Lakini pili, nataka nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba sio rahisi kutambua jina peke yake ukasema huyu anatoka Zanzibar na huyu anatoka Tanzania Bara. Kwenye zile fomu ambazo zinaombwa kwa ajili ya udahili, kitu kimoja tu ambacho kinaombwa kuonyeshwa nacho ni utaifa. Kwa sababu Vyuo Vikuu ni *Universal*, tunataka kufahamu kama huyu ni Mtanzania, huyu ametoka Burundi, ametoka Kenya, ametoka sehemu gani, lakini hatuna sehemu ambayo inasema utaje kama unatoka Tanzania Bara au unatoka Tanzania Visiwani.

Lakini vilevile kwa kutizama *address* peke yake haisaidii kwa sababu unaweza kukuta mtu ameandika *address* ya Zanzibar lakini mtu huyu ni Mtanzania bara. Vilevile, unaweza kukuta mtu ana *address* ya Bukoba, lakini vilevile huyu mtu anatoka Tanzania Visiwani. Kwa hiyo, hii haiwezi kutofautisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nafasi, ni kwamba katika udahili wa Vyuo Vikuu kitu kinachoangaliwa ni sifa za mwombaji katika kozi anayotaka kuingia. Hakuna upendeleo kwa maana ya mgawanyo kati ya Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara. Ni kazi ya ushindani.

Lakini hata hivyo, katika ngazi nyingine Vyuo Vikuu katika udahili huwa vinatizama jinsia na pale hutolewa upendeleo maalum pale wanapokuwa sawa mwanaume na mwanamke, basi jinsia ya kike ndio inachukuliwa, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. YAHAYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa chombo hiki ni cha Muungano na Muungano huu unaeleweka kwamba baina ya Tanzania Bara na Zanzibar na mara nyingi katika harakati zetu tuna wajibu wa kuwakilisha kati ya Zanzibar na Tanzania Bara; Serikali haioni kwamba sasa umefika wakati muafaka wa kuelewa ili kuondoa malalamiko na kuwa na manung'uniko kwamba, ieleweke kwamba katika wanaojiunga katika Vyuo hivi, huyu anatoka Zanzibar na huyu anatoka Tanzania Bara ili kuleta uwiano?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi na kama alivyoeleza Waziri wa Elimu ya Juu, ukweli ni kwamba suala la kitaalam haliwezi kuwa suala la mgao, ni suala la ushindani. Narudia kusema kwamba, hatuwezi kuwa na *quarter system* katika Elimu ya Juu.

Kwa hiyo, naomba akubali kwamba tutaendelea kufuata vigezo vya kitaaluma na ushindani katika taaluma na kwa hali hiyo, mimi nafikiri aridhike kwa sababu Wazanzibar wengi sana wanakuja kusoma Chuo Kikuu Dar es Salaam na Vyuo vingine vya huku Tanzania Bara na wengi nimesoma nao na walikuwa wazuri. Kwa hiyo, waendelee kukazana ili waweze kupata nafasi. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 57

**Mfuko wa Mikopo ya Wanafunzi**

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tanzania Zanzibar kuna Vyuo Vikuu visivyopungua vitatu na kwa kuwa uko Mfuko wa Mikopo ya Wanafunzi ambao unalenga kuwasaidia vijana wa Kitanzania hasa wale wasio na uwezo:-

(a) Je, katika Muundo wa Bodi ya Mikopo ya wanafunzi, kuna Wawakilishi wangapi toka Tanzania Zanzibar?

(b) Je, ni wanafunzi wangapi walipatiwa mikopo kati ya mwaka 2003-2004 na 2004-2005 na kati ya hao ni wangapi wametoka Zanzibar na ni vijana wa Vyuo gani?

(c) Je, ni wanafunzi wangapi wanaosoma nje ya Tanzania wamepatiwa mikopo na kati ya hao ni wangapi ni wanawake?

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Kwa mujibu wa Sheria Na.9 ya mwaka 2004 sehemu ya II, aya ya 5(i) kinaeleza kuwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia atawateua Wajumbe wasiopungua tisa (9) na wasiozidi kumi na nne(14) kama ifuatavyo:-

(a) Mwenyekiti;

(b) Mkurugenzi wa Elimu ya Juu;

(c) Mjumbe anayewakilisha Wizara ya Elimu ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;

(d) Mjumbe mmoja wa Wizara ya Fedha;

(e) Mkurugenzi wa Elimu na Ufundi;

(f) Mwanasheria aliyebobea kutoka katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu;

(g) Mwakilishi kutoka Tume ya Ajira;

(h) Mwakilishi wa Mashirika ya Fedha;

(i) Mwakilishi wa Vyuo vya Elimu ya Juu vya Umma;

(j) Mwakilishi wa Vyuo vya Elimu ya Juu vya Binafsi;

(k) Mwakilishi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi;

(l) Mwakilishi wa Wizara ya Fedha - Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;

(m) Mwakilishi wa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu vya Umma; na

(n) Mwakilishi wa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu vya Binafsi.

Baada ya maelezo hayo mafupi, sasa ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mbunge wa Matemwe, lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Bodi inao Wajumbe wawili waliotajwa kisheria wanaotokea Zanzibar na kwa nyongeza, kwa kipindi hiki, Mwakilishi wa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu vya Binafsi kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar anatokea Zanzibar.

(b) Mheshimiwa Spika, Wanafunzi waliopata mikopo katika mwaka wa 2003/2004 ni 15,668 na 2004/2005 ni 17,020.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema Fomu za Maombi ya Mikopo kwa muda wote hatuhitaji mwombaji ataje sehemu gani ya Tanzania anakotoka iwe ni Tanzania Visiwani au Bara au Mkoa. Kinachoulizwa ni anuani ya kudumu ya mwombaji. Hivyo mwombaji anaweza kuwa anatoka Zanzibar akajaza anuani ya kudumu ya Singida au mwombaji anayetoka Bara akajaza anuani ya kudumu ya Zanzibar, hivyo ni vigumu kwa mwombaji kutambulika kuwa anatoka Zanzibar ama la kwa sababu tu ya anuani yake.

Mkopo wa chakula na malazi uliotolewa wakati huo uliwalenga tu Watanzania wote waliokuwa na udhamini wa Serikali katika Vyuo vyote nchini. Hivyo ni dhahiri kuwa wanafunzi wote kutoka Zanzibar waliokuwa wanasoma chini ya udhamini wa Serikali ama ya Muungano na au ya Zanzibar kwa mwaka 2003/2004 na 2004/2005 kwenye Vyuo vya Elimu ya Juu walipewa mkopo.

(c) Wanafunzi wanaosoma nje ya nchi waliopata huduma ya mikopo mwaka 2005/2006 ni 1,056 na kati yao wanawake ni 266.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini nina swali moja la nyongeza. Nini matazamio ya Wizara ili kuongeza idadi ya wanafunzi katika mwaka 2005/2006 katika Vyuo hivi?

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, Wizara ina mipango ya kuongeza idadi ya wanafunzi wa vyuo vikuu kutokea idadi tuliyonayo sasa vyuo vikuu vya umma ambayo ni 36,770 kufikia katika miaka mitano ijayo 73,150, lakini yote yatategemeana na raslimali ambayo itakuwa imepatikana kwa ajili ya kupanua Elimu ya Juu.

Pamoja na hayo, Wizara itaendelea kuwahamasisha wawekezaji katika Sekta hii ikiwa ni pamoja Mashirika ya Dini na Mashirika mengine ambako sasa hivi wana Vyuo jumla ya 19 ambavyo vimeongeza idadi ya wanafunzi 5176 na idadi hii imeongezeka kutoka ile idadi ambayo tulikuwa nayo wakati Wizara hii inaanzishwa mwaka 1990, Novemba ambayo idadi hiyo ilikuwa ni wanafunzi 4,850 na sasa imefikia 36,870. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha. Tulibakiza maswali miwili ambayo nitayapa kipaumbele katika *Order Paper* ya Jumatatu.

Sasa napenda pia kukumbusha kwamba hatutakuwa na Kikao kwa maana ya kuendeleza Kikao cha Bunge leo jioni, kwa sababu kama ilivyotangazwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano analihutubia Taifa kutoka Dodoma ingawa atakuwa anaongea katika Ukumbi wa Kilimani na wakati Wazee na Viongozi wa Dodoma. Tulishauriana na Kiongozi wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni na tumekubaliana kwamba ni vizuri na ni heshima kutokuwa na matukio miwili ya Kitaifa yanayoendelea kwa wakati mmoja. Ndiyo maana tunaomba kwamba Wabunge wote twende, tumekaribishwa kuweza kumsikiliza Rais moja kwa moja anapolihutubia Taifa leo Saa 10:00 jioni.

Kwa maana hiyo, Ofisi ya Spika imeandaa usafiri wa mabasi kama kawaida kutokea hapa saa 9:00 jioni ili kutoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge kuweza kuwahi na kuwa mahali pao wameketi kwani wametengewa mahali maalum pa kuketi. Basi ni vizuri tuwahi wale wanaojitegemea na wale watakaotumia usafiri wa mabasi tuwe tumefika pale saa 9:00 jioni ili kuweza kuketi.

Matangazo mengine ni kwamba kesho Jumamosi saa 3:00 asubuhi kutakuwa na Semina kwa Waheshimiwa Wabunge wote itakayoendeshwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano yaani *Tanzania Communications Regulatory Authority.* Hii ni muhimu sana katika kuelewa haya masuala ya mawasiliano, simu za mkononi na kadhalika.

Aidha, kutakuwa na Semina nyingine pia kwa Waheshimiwa Wabunge siku ya Jumapili tarehe 02/04 itakayoanza saa 5:00 asubuhi. Semina hiyo ni ya *TASAF,* nayo ni muhimu sana. Kila Wilaya katika nchi yetu sehemu zote za Muungano kuna *TASAF,* basi ni vizuri tuje tusikilize ili tuulize maswali tupate ufahamu wa kina kuhusu mradi huu muhimu wa Kitaifa.

Wajumbe wote wa Kamati za Uwekezaji na Biashara, Kamati mbili hizo na Miundombinu ya tatu, ni mbili nadhani, leo Uwekezaji na Biashara ni moja na Miundombinu leo mara baada ya uchaguzi wa Wawakilishi wa Mabaraza ya Vyuo mbalimbali wakutane katika Chumba Na.428 ghorofa ya nne kwa ajili ya kukutana na wawekezaji wa Mradi wa Mchuchuma Wilayani Ludewa tafadhali mnaombwa wote kuhudhuria. Pamoja na ombi lingine kwamba Waheshimiwa Wabunge wote wanaoguswa na mradi huu yaani Mikoa ya Iringa na Ruvuma na wengine wowote ambao wanaweza kwenda kusikiliza maendeleo ya mradi mkubwa wa Mchuchuma wa Makaa ya Mawe, kwa hiyo, ni Ukumbi Na. 428 mara baada ya Bunge kuahirishwa asubuhi hii.

Tangazo lingine ni kwamba leo baada ya Bunge kuahirishwa kutakuwa na Kikao cha Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* kwenye Chumba Na. 227 ghorofa ya pili jengo la Utawala mara baada ya kuahirishwa Bunge asubuhi hii.

Tangazo lingine pia ni kwamba, Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya *APNAC* wanaombwa kukutana na Balozi wa Marekani Chumba Na.113, sasa hii imesema saa 4:00. Lakini kuna uchaguzi, sasa itakuwa labda baada ya kuahirisha Bunge.

Baada ya matangazo hayo, sasa namwita Katibu atupe utaratibu wa shughuli inayofuata.

## UCHAGUZI WA WAJUMBE KWENYE BODI ZA TAASISI ZA ELIMU YA JUU

**ND. DAMIAN S. L. FOKA – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, shughuli inayofuata ni uchaguzi wa Wajumbe kwenye Bodi za Taasisi za Elimu ya Juu.

**SPIKA:** Utaratibu.

**ND. DAMIAN S. L. FOKA – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nilitoa tangazo kwa nafasi hizi za Wajumbe wa Taasisi zifuatazo:- Bodi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya, Bodi ya Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere na Bodi ya *Tanzania Commission for Universities.*

Mpaka jana saa 10:00 jioni maombi ya wafuataο ndio ambao wameomba kugombea nafasi. Kwa Chuo cha Mbeya, amepatikana au ameomba mtu mmoja tu, naye ni Dr. Binilith S. Mahenge. Utaratibu tunaoufuata ni kwamba anapita bila kupingwa. *(Makofi)*

## BODI YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA MBEYA (MIST)

**SPIKA:** Basi Waheshimiwa Wabunge, kwa kauli hiyo tunampokea Dr. Binilith Mahenge kuwa ndiyo Mwakilishi Mbunge katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya.

**SPIKA:** Ahsante sana. Basi, kwa niaba ya Bunge zima nakupongeza kwa ushindi huu. *(Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge Alisimama na kuonekana )*

## BODI YA CHUO CHA KUMBUKUMBU CHA MWALIMU NYERERE

**ND. DAMIAN S. L. FOKA – KATIBU WA BUNGE:** Nafasi inayofuata ni kwa ajili ya Mjumbe kwa Bodi ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, naye aliyeomba ni mmoja ambaye ni Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa makofi hayo ni dhahiri kwamba Mheshimiwa Mwanri amekubalika na Bunge zima kuwa ndiye Mwakilishi wetu katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Nakupongeza sana kwa hilo.

*(Hapa Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri Alisimama na kuonekana)*

**ND. DAMIAN S. L. FOKA – KATIBU WA BUNGE:** Unaofuata ni uchaguzi kwa ajili ya *Mzumbe University.* Aliyeomba hapa ni mmoja, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji. *(Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji Alisimama na Kuonekana)*

**SPIKA:** Hapo napo nadhani tumakubaliana kwa utaratibu mzuri kabisa tuliouweka ndani ya Bunge hili kwamba unapopata mgombea mmoja, basi anapita bila kupigiwa kura. Kwa hiyo Dr. Haji Mwita Haji nakupongeza sana, wewe sasa ndiye Mwakilishi wetu katika Tume ya Vyuo Vikuu vya Tanzania, yaani Tanzania *Commission for Universities (Makofi)*

**ND. DAMIAN S. L. FOKA – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba tumemaliza shughuli ya uchaguzi kwa ajili ya Uwakilishi wa Bodi katika sehemu hizo tatu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nadhani ni heshima tutumie muda mfupi sana kwa hawa Waheshimiwa tuliokwishawachagua. Sasa hivi kama ilivyokawaida yetu, wapite hapa mbele waseme kwa ufupi sana maneno ya kushukuru tu halafu baada ya hapo tuendelee na shughuli nyingine. Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge karibu halafu Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri ajiandae na Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, lakini mngetoka kabisa muwe karibu.

**HOTUBA YA SHUKRANI**

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nimesimama hapa kwa unyenyekevu mkubwa sana kuwashukuru sana kwa imani mliyonipatia ili niwawakilishe katika Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya. Nawashukuru sana. Nami naahidi kuwawakilisha kikamilifu na ninaamini nina uwezo wa kuliwakilisha Bunge hili Tukufu katika Chuo hiki. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Baraza la Mawaziri naomba nichukue nafasi hii kwa unyenyekevu mkubwa sana kuwashukuruni sana kwa heshima kubwa ambayo mmenipa. Kama mnavyojua na kama nilivyojieleza katika karatasi ile ya maelezo, nimefanya kazi Kivukoni kwa miaka 11 na nilipoona kwamba kuna nafasi hii,

nikaomba nafasi hiyo kwa ajili ya kutumia uzoefu wangu katika Chuo hiki cha Mwalimu Nyerere cha Kumbukumbu ya Baba wetu wa Taifa ambaye amefanya kazi kubwa.

Kwa hiyo, ni heshima kubwa sana kwamba Wabunge wenzangu, mmekubali kwamba nirudi Kivukoni na ninataka niwathibitishie kwamba sitawaangusha, nitafanya kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia, zile *political economy* zinazopigwa hapa sehemu yake ni katika hizo harakati za Kivukoni.

Nawashukuru sana na Mungu awabariki. *(Makofi)*

**MHE. DR. HAJI M. HAJI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wenzangu: Nimesimama hapa mbele yenu kutoa shukrani zangu za dhati kwenu kwamba mbali na kwamba pengine hamkuelewa, lakini mmeelewa kwa sababu kwa roho zenu ziliwapa fursa kuona kwamba atakayechagua nafasi hii atakuwa mtu anayefaa.

Kwa hiyo, natoa shukrani za dhati kwenu kwamba baada ya kwamba roho zenu zimeamua hivyo kwamba atatokea mtu anayefaa na nikachaguliwa mimi leo hapa kuwa mbele yenu kuja kuwawakilisheni katika *Commission of the Universities of Tanzania.* Kwa hiyo, natoa shukrani na kuahidi kwamba nitakuwa tayari na uwezo nina hakika ninao. Kwa hiyo, niwaambie wale Wazanzibar kwamba Mwita hii ni Mwita ya Zanzibar na uwezo huo upo na tutafanya kazi kama inavyotakiwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, shughuli za asubuhi hii sasa tumezikamilisha na kabla sijaahirisha Bunge ningependa kukumbusha tu kwamba Waheshimiwa wafuatao wameomba kuchangia kwenye hoja ya Benki Kuu ambayo tutaendelea nayo Jumatatu. Nawakumbusha tu kwa sababu tunaingia katika *weekend,* kwa hiyo ni vizuri wakajua.

Waheshimiwa hao ni Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Susan A.J. Lyimo, MheshimiwaJenista J. Mhagama, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Martha Moses Mlata na Mheshimiwa Anna R. Lupembe kwa saa 4:30 asubuhi siku ya Jumatatu, tarehe 3 Aprili, 2006.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wabunge, sasa naliahirisha Bunge hadi Siku ya Jumatatu tarehe 03/04//2006 saa 3:00 asubuhi hapa Ukumbini.

*(Saa 04:45 Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu tarehe 03 Aprili, 2006 Saa 03:00 Asubuhi)*